# Ulinganishi kati ya mofu na mofimu katika mofolojia ya lugha ya  Kiswahili

■ Dr.Abdalla M. Aghel *

● Received: 15/02/2026 ● Accepted:04/03/2026

■ **Ikisiri:**

Utafiti huu  unaohusu Ulinganisho kati ya mofu na mofimu katika mofolojia ya lugha ya  Kiswahili unachunguza na kuchambua dhana za lugha za "mofu" na "mofimu." Istilahi hizi zinatokana na istilahi za Kiingereza zinazotumika sana katika uchanganuzi wa lugha, hasa katika kiwango cha mofolojia. Kwa kuzingatia umuhimu wake muhimu katika isimu na mkanganyiko unaotokea mara nyingi unapotumiwa na wanafunzi na walimu wengi wa Kiswahili, pamoja na Kiingereza (ambacho kilitoka), utafiti huu unashughulikia dhana hizi.

●**Istilahi za Msingi: mofu, mofimu, isimu, mofolojia.**

■ **المستخلص:**

يتناول هذا البحث دراسة وتحليل المفاهيم اللغوية (موفو ومورفيم) وهي مصطلحات مشتقة من مصطلحات انجليزية الأكثر استخداما في التحليل اللغوي،ب وخاصة على المستوى الصرفي، ونظرا لأهميتها البالغة في علم اللغويات وما يقع من اختلاط في المفاهيم عند استخدامها من العديد من الطلاب والقائمين على تدريس اللغة السواحيلية وكذلك اللغة الانجليزية التي نشأت منها.

● **الكلمات المفتاحية:** وحدة لغوية (مجسدة)، وحدة لغوية، علم الصرف، علم اللغة.

E-maiI:ab.aghel@uot.edu.ly

1.0 **Utangulizi :**

Lugha ya Kiswahili ni lugha ya Kiafrika yenye kanuni tofauti za isimu,fonolojia,

fonetiki na mofolojia ya aina zote za maneno ya lugha yaani vihusishi, vielezi, vitenzi, nomino, viambishi, viunganishi, viwakilishi na vivumishi.

Dana muhimu za kimofolojia na kifonolojia kama vile viambishi, mzizi, alofoni, shina, mofu, mofimu, alomofu, fonimu.

Na dhana za mofu na mofimu ndizo ambazo hutumiwa sana kwa uchambuzi wa kiisimu hususani katika kiwango cha mofolojia, Na istilah hizi zote zimetoholewa kutoka istilahi za kiingereza (Mgullu1999), yaani:

a- Mofu kutoka morph.

b- Mofimu kutoka morpheme.

Kwa kusoma sarufi ya Kiswahili, tulijifunza kwamba Kabla ya kuasisiwa kwa sarufi zalishi, yaani kipindi cha sarufi mapokeo, uchanganuzi wa sarufi uliishia katika darajia ya neno,Kwa maana hiyo, vipashio vinavyounda neno havikuchanganuliwa kabisa. Hata hivyo, katika kipindi cha sarufi miundo uchanganuzi ulipiga hatua na mofimu zikaanza kuchanganuliwa, Kwa msingi huo, mofimu ilitumika kurejelea kipashio cha mwisho kabisa cha uchanganuzi. Kwa mfano, kitenzi: (anasoma) kinavunjwavunjwa katika vijenzi: (ana-som-a) ambavyo haviwezi kuchanganuliwa zaidi bila kuharibu maana na umbo la kijenzi husika. Kutokana na ufafanuzi huo, mofimu ilielezwa kuwa ni kipashio kidogo kabisa katika lugha chenye maana kisarufi au kileksika (Booij, 2007).

Kwa ujumla, mofolojia kabla ya sarufi zalishi iliwakilisha umbo na maana; yaani, mofimu ni umbo na maana. Miongoni mwa wanazuoni wanaochukua mtazamo huu ni (Nida,1941) na Richards ( 1985).

Mkabala wa sarufi zalishi uliibuka mnamo Karne ya 20 ambapo dhana za mofu na alomofu zilianza kutumika katika uchanganuzi wa kisarufi. Katika kipindi hicho kulitokea uhamaji wa maana ya mofimu kwenda kwenye mofu na mofimu kupewa maana mpya (Matthews, 1997). Maana iliyotumika kurejelea mofimu, yaani kipashio kidogo kabisa cha lugha chenye maana kisarufi au kileksika ikatumika kurejelea mofu na mofimu ikapewa maana

mpya ambayo ni kipashio dhahania cha umbo ulani ambacho kinaweza kuwakilishwa na mofu tofautitofauti katika mazingira anuwai (Hartman, 1972). Aidha, Lightner (1975) anaeleza kuwa mofu imo katika utendaji lakini mofimu ni dhana dhahania iliyomo akilini mwa mtumiaji wa lugha ambayo ni sehemu ya umilisi wake kuhusu lugha husika. Kwa hiyo, mofimu ni tafsiri ambayo mtu huijenga akilini mwake kuhusu umbo fulani la neno, yaani mofu. Kwa hakika, fasili hii ndiyo yenye mashiko katika kutofautisha dhana ya mofu na mofimu.

## 2.0 **Suala la utafiti**

Utafiti huu kuhusu mofu na mofimu katika lugha ya Kiswahili unaibua mswali muhimu sana :

a- Je, kuna tafauti gani kati ya mofu na mofimu katika lugha ya Kiswahili?

b- Je, kuna ufanana baina ya mofu na mofimu?

c- Tunajuaje jinsi ya kutofautisha kati ya mofu na mofimu?

## 3.0 **Malengo ya utafiti**

Utafiti huu umejengwa na malengo ya aina mbili ambayo ni lengo kuu na malengo mahususi.

### 3.1 Lengo kuu la utafiti

Lengo la utafiti huu ni kuchunguza tofauti na mfanano uliopo baina ya mofu na mofimu.

### 3.2 Malengo Mahususi

* kubainisha mofu na mofimu katika lugha ya Kiswahili.

* kubainisha jinsi ya kutofautisha kati ya mofu na mofimu.

* kulinganisha kazi za mofu na mofimu katika sentensi za Kiswahili.

## 4.0 **Umuhimu wa utafiti**

Utafiti huu unatarajiwa kuwa na faida kubwa kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili na wa walimu ambao wanafundisha lugha ya Kiswahili,pia utafiti huu utakuwa muhimu sana kwa wasomi wote wa lugha ya Kiswahili, na uatakuwa marejeleo muhimu wakati wa kuandika kuhusu sarufi ya Kiswahili.

### 5.0 Mbinu za Utafiti na Nadharia

Utafiti huu ulitumia hojaji na ushuhudiaji kama mbinu ya kukusanya data kutoka kwa watafitiwa, mtafiti alipanga data kutokana na maudhui na makundi ya wasailiwa yanayofanana kisifa.

Mtafiti alikuwa makini katika kueleza, kufananua, kuhakiki na kutafsiri data alizozipata katika utafiti huu kwa kutumia mkabala wa kimaelezo, na pia mtafiti alikuwa makini katika kueleza, kufafanua, kuhakiki na kupanga data katika makundi kwa mujibu wa maswali ya utafiti, na mkabala mmoja ulitumika katika ukusanyaji na uwasilishaji wa data za utafiti huu, mkabala huyo ni mkabala wa kimaelezo.

Utafiti huu unaongozwa na nadharia ya umbo upeo, iliyoasisiwa na Prince na Smolensky (1993).

### 6.0 Mofu :

Mofu ni istilahi ambayo imetoholewa kutoka istilah morph kutoka lugha ya kiingereza.

mofu ni istilahi ambayo imetoholewa kutoka istilah morph kutoka lugha

ya kiingereza

Ni kipashio kidogo cha lugha chenye maaana katika lugha (Platt 1985).

Mofu ni kipashio cha kimofolojia kinachowakilisha mofimu(Tuki 1990).

Ni kipashio kidogo kabisa cha lugha kinacho beba au kinachostiri maana.

### 6.1 Dhana za mofu:

Katika mofolojia, ni muhimu kutofautisha kati ya wezo lililoko akilini (dhana), na kile kinachoandikwa au kutamkwa (umbo halisi), ikiwa mofimu ni dhana dhahania iliyoko akilini mwa mzungumzaji, mofu ni kiwakilishi halisi cha nje na kinachoshikika cha mofimu hiyo katika matamshi au maandishi, na Sifa muhimu zinazopambanua dhana ya mofu ni:

1- Mofu haiwezi kugawika katika vipengele mbalimbali.

2- Hudhirika kimofolojia na kiothografia.

3- Mofu ni sehemu halisi ya neno.

### 6.2 Aina za mofu:

Kuna aina tano za mofu, ambazo baadhi yake ni huainishwa kwa kuzingatia hasa vigezo viwili : mofolojia ya mofu na maana zinazowakilishwa na mofu, unapotumia kigezo cha mofolojia (maumbo ya mofu) tunaona kwamba kuna aina mbili za mofu ni: mofu changamano, mofu, kapa, na unapotumia kigezo cha maana zinazowakilishwa na mofu, tunazo mofu za aina tatu: mofu huru, mofu funge, mofu tata (Mgullu 1999).

· **Mofu huru:**

Mofu huru ni zile mofu ambazo zinaweza kukaa peke yake kama maneno kamili yenye maana inayoweza kuelekwa bila kusaidiwa na mofu nyingine(Weber1985).

Mara nyingi mizizi ya baadhi ya maneno ndiyo ambayo huwa na uwezo wa kukaa peke yao, na ikawa maneno kamili yanayojitosheleza kwa mfano:

| | | | |
|---|---|---|---|
| *Nomino:* | | | |
| - Mimi | - paka | - baba | - ndege |
| *Vivulishi:* | | | |
| - Zuri | - ghali | - baya | - safi |
| *Viwalilishi:* | | | |
| - Mimi | - wewe | - sisi | - wao |
| *Vielezi:* | | | |
| - Leo | - jana | - juzi | - upesi |
| *Vitenzi:* | | | |
| - Jibu | - cheza | - soma | - andika |
| *Viunganishi:* | | | |
| - Pia | - halafu | - na | - bado |
| *Vihusishi:* | | | |
| - Juu | - chini | - nyuma | - mbele |

● **Mofu tata:**

ni mofu ambazo huwa na maana zaidi ya moja, na kwa tafsiri ya Weber, mofu tata ni kipashio cha kiisimu huitwa tata wakati ambapo kipashio hicho kinaweza kupewa maana zaidi ya moja ( Webar 1985. Mfano:

| alimandikia |
|---|
| **(a)** Mofu (**li**) mofu (**m**) mofu (**andik**) mofu (**i**) mofu (**a**) mofu. |
| Katika kitenzi hiki (alimandikia) kuna mofu sita, lakini (**i**) ambayo ni mofu tata. |

● **Mofu funge**

Ni mofu ambayo haiwezi kukaa peke yake ikawa neno kamili, na maana zake hutegemea na muktadha wa mofu.

“ mofu funge ni mofu ambayo haiwezi kutumiwa peke yake kama neno kamili, lililo na maana yake bainifu, bali (daima) hutumiwa kama kiambishi tu kinachoambatana na mzizi au viambishi vingine ili kulikamilisha neno( Hartman 1972). Kwa mifano:

| Mwalimu: |
|---|
| (**Mw**) ni mofu funge. |
| Kucheza: |
| (**Ku**) ni mofu funge, na (**a**) pia ni mofu. |

● **Mofu changamano**

Mofu changamano ni aina mojawapo ya mofu ambayo imepewa jina kwa kuzingatia zaidi muundo wake, na huundwa kwa kuweka pamoja angalau mashina hayo yanaweza kutenganishwa na kila moja likawa ni neno kamili, kwa mfano:

| Mwanachama: |
|---|
| (**Mw**) ni mofu fungo |
| (anachama) ni mofu changamano imeundwa kwa mizizi miwili ya manano. |

- **Mofu kapa**

Mofu kapa ni kipashio cha kidhahania ambacho kimeundwa kwa madhumuni ya uchunguzi lakini hakijitokezi dhahiri (Tuki, 1990)

Mofu kappa ni mofu ambayo haina umbo lakini huwakilisha maana, itafaa tutumie mfano wa mofu za idadi ya umoja na wingi tukichunguza ruwaza ya viambishi awali vya umoja na wingi katika lugha ya Kiswahili na tunaweza kuzingawa nomino za Kiswahili katika makundi makuu manne (Mgullu, 1999) yaani:

a- Nomino zilizo na viambishi bayana vya idadi ya umoja na wingi:

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **ki**tabu | **vi**tabu |

b- Nomino zilizo na kiambishi awali cha umoja tu, cha wingi hakipo:

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **u**kuta | kuta |

c- Nomino zilizo na kiambishi cha wingi tu, cha umoja hakipo:

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| debe | **ma**debe |

d- Nomino zisizo na kiambishiawali cha idadi hata moja:

| Baba | Mama |
|---|---|
| Samaki | kalamu |

**7.0 Mofimu :**

Mofimu ni kipashio kidogo kabisa katika lugha chenye maana na zaidi.

Nadharia ya sarufi zalishi ilisema kuwa mofimu ni maana inayositiriwa ndani ya mofu(Mohamed 1986).

Ni kipashio kidogo kabisa dhania cha kisarufi kilicho na maana (Crystal1971).

**7.1 Aina za mofimu:**

kuna aina mbili za mofimu nazo ni: mofimu huru, mofimu tegemezi.

1. **Mofimu huru:**

Mofimu huru ni silabi moja au zaidi yenye maana kamili ya neno na inaweza kujisimamia yenyewe bila msaada wa viambishi au silabi nyingine, na aghalabu mofimu huru huwa nomino, vielezi ua vivumishi visivyochukua viambishi vya ngeli.

Kwa mfano:

Mwalimu, kazi, chumba.

2. **Mofimu Tegemezi:**

Mofimu tegemezi ni mofimu ambazo huhitajia viambishi au mofimu nyingine tegemezi ili kuleta maana iliyokusudiwa , na mofimu hizi hujumuisha hasa mzizi wa neno au shina la kitenzi, nomino, vivumishi, vielezi ambavyo vinahitaji viambishi viwakilishi vya ngeli ili kutoa maana iliyokusudiwa.

Kwa mfano:

mchezaji

( **m**) ni mofimu ya ngeli ya M-WA kwa umoja.

(**chez**) ni mzizi wa neno.

(**a**) ni kiisho cha kitenzi.

(**ji**) ni inaonyesha kazi au mazoea.

**7.2 Dhana za mofimu:**

Mathews (1997) anaeleza kuwa dhana ya mofimu ni changamani, jambo ambalo huongeza utata wa kuipambanua katika lugha. Aidha, historia inaonesha kuwa istilahi mofimu ndiyo ilianza kutumika kabla ya mofu na alomofu (Crystal, 1971) na anaeleza kuwa wakati wa sarufi mapokeo uchambuzi wa kiisimu uligawanya vipashio vidogovidogo kama vile vishazi, virai na hatimaye neno. Kwa hiyo, viambajengo vinavyojenga neno havikuweza kuchanganuliwa katika kipindi hicho. Lakini baadaye katika Karne ya 18 na 19 ilibainika kuwa palikuwa na haja ya kuchanganua

viambajengo vinavyojenga neno. Wakati huo ndipo istilahi mofimu ilipoanza kutumika na mofu ilianza kutumika Karne ya 20 hasa baada ya kuasisiwa kwa sarufi zalishi. Kwa maelezo hayo, dhana ya mofimu ina sura mbili zinazotofautiana sana, yaani mofimu kabla ya kuasisiwa kwa sarufi zalishi na mofimu baada ya kuasisiwa kwa sarufi zalishi (Mathews, 1997).

a- **Dhana ya mofimu kabla ya sarufi zalishi:**

Kabla ya kuasisiwa kwa sarufi zalishi uchanganuzi wa sarufi uliishia katika daraja ya neno, na vipashio vinavyounda neno havikuchanganuliwa kabisa, hata hivyo, katika kipindi cha sarufi miundo uchanganuzi ulipiga hatua na mofimu zikaanza kuchanganuliwa, na mofimu ilitumika kurejelea kipashio cha mwisho kabisa cha uchanganuzi( Ndumiwe, Jasson 2022).

Wataalamu wa lugha ya Kiswahili ( wanaisimu) walipoona umuhimu wa kuwa na kipashio kidogo zaidi ya neno katika uchambuzi,mara waliibuni na kuanza kutumia dhana ya mofimu, na walichambuzi kila neno na herufi hadi kwenye kiwango cha mofimu.

Kwa mfano sentensi kama: *Ali anacheza mpira*, ingechambuliwa sentensi imegawanywa katika sehemu kuu mbili yaani:

a- Kiina ( Ali ) b- Kiarifu ( anacheza mpira ).

Na ukichambuzi sentensi hizi baada ya kuasisiwa sarufi zalishi utaona kwamba sentensi ni mfululizo wa mofimu saba :

Kiima kina nomino moja (Ali) na nomino hii ina mofimu moja tu ambayo ni (**Ali**) , na Kiarifu kina kitenzi ( alicheza) na kitenzi hiki kina mofimu nne (**a** – **na** – **chez_ a**), na nomino (mpira) ina mofimu mbili (**m- pira**).

b- **Dhana ya mofimu baada ya kuasusiwa kwa sarufi zalishi:**

Katika uchambuzi wa mofolojia ya lugha Dhana muhimu mbili ziliingizwa baada ya kuasisiwa kwa sarufi zalishi, dhana hizo ni mofu na alomofu, na mofu ilichukua maana iliyokuwa imepewa mofimu na mofimu ikapewa maana mpya, fasili mojawapo inayotoa hii maana mpya ya mofimu ni ile ya Hartman(1972) ambaye anasema kuwa: " mofimu ni kipashio dhahania cha umbo fulani ambacho kinaweza kuwakilishwa na mofu tofauti tofauti katika mazingira anuwai. Kwa mfano:

Mohamed anaishi Libya :

| Mofu | Mofimu |
|---|---|
| Mohamed | Mtu<br>Idadi : mmoja<br>Jinsia: mwanaume |
| a | Kipatanishi<br>Nafsi ya tatu<br>Idadi : mmoja |
| na | Njeo: sasa<br>Hali : kuendelea |
| ish | Mzizi wa kitenzi |
| i | Kiambishi tamati<br>Kauli ya kutenda<br>yakinishi |
| Ø( kapa) | Idadi ya moja |
| Libya | Mzizi wa nomino Nshi |

Mofimu hapa si maumbo ya maneno bali ni maana tunazozichuja akilini mwetu.

**8.0 Tofauti ya mofu na mofimu:**

Mofu ni umbo ambalo huweza kuandikwa na huweza kutamkwa.

Mofimu ni dhana iliyo akilini ambayo ni tafsiri ya maana inayowakilishwa na mofu.

Mfano:

Katika neno a – na – chez – a

(**a**) ya kwanza ni mofu, tunaiona kwa vile imeandikwa, pia yaweza kutamkwa tukaiskia.

Kwa maana zaidi mofu ni kipashio halisi kinacho weza kutamkika na kuandikika wakati mofimu ni kipashio dhahania.

Mofu ni umbo linalostiri maana katika neno,lakini mofimu ni maana

inayositiriwa na maumbo.

**Tofauti Kuu kati ya mofu na mofimu:**

*1*. Mofu inaweza kuwa na maana au isiwe na maana, lakini mofimu lazima iwe na maana.

*2*. Mofu ni kipashio cha sauti, wakati mofimu ni kipashio cha maana.

*3*. Mofimu ni mofu yenye maana, lakini si kila mofu ni mofimu.

**Mfano wa Tofauti**

Neno “msomaji”:

Mofu: m-so-ma-ji

Mofimu: m- (anaefanya), -soma- (shina la neno), -ji (mhusika)

Mfano mwingine wa tofauti kati ya mofu na mofimu:

Neno “ mchekaji”

Mofu: m-che-ka-ji

Mofimu: m- (anaefanya), -cheka- (shina la neno), -ji (mhusika)

Kwa hiyo, mofimu ni mofu yenye maana, lakini mofu inaweza kuwa na maana au isiwe na maana.

**9.0 Uhwiano baina ya mofu na mofimu:**

Uhwiano baina ya mofu na mofimu katika isimu-lugha (mofolojia) ni wa utegemezi, ambapo mofu ni umbo la nje linaloonekana au kutamkwa, huku mofimu ikiwa ni dhana ya maana iliyo akilini. Wao ni pande mbili za sarafu moja katika uchambuzi wa muundo wa maneno.

Maana yake hapo kuna uhusiano mkubwa sana kati ya mofu na mofimu maana ni vipashio ambavyo utegemeana sana katika sarufi, na Mofu na mofimu vyote ni vipashio vya kileksika.

Pia mofu na mofimu ni aina ya sarufi yaani sarufi maumbo ni mofu na sarufi maana ni mofimu.

**10.0 Hatimisho**

Utafiti huu ulilinganisha kati ya mofu na mofimu katika mofolojia ya lugha ya Kiswahili, Na matokeoya utafiti huu yanatuonesha kwamba kuna tofauti

kati ya mofu na mofimu, na tofauti hii inaweza kufupishwa katika mambo yafuatayo:

Mofu inaweza kuwa na maana au isiwe na maana, lakini mofimu lazima iwe na maana.

Mofu ni kipashio cha sauti, wakati mofimu ni kipashio cha maana.

Mofimu ni mofu yenye maana, lakini si kila mofu ni mofimu.

Uhusiano uliopo baina ya mofu na mofimu ni ule wa kiashiria na kiashiriwa. Mofimu ni dhana dhahania (inayokaa akilini), wakati mofu ni utekelezaji au umbo halisi la dhana hiyo katika maandishi au matamshi.

Aidha utafiti unaonesha kwamba, katika mofolojia ya lugha ya Kiswahili dhana za mofu na mofimu zinatofautiyana, na umebainisha dhima za mofu, mofimu katika mofolojia ya lugha ya Kiswahili.

## ■ Marejeleo


- Mgullu, R.S. (1999). Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia, na Mofolojia ya Kiswahili. Nairobi: Longhorn.
- Booij, G. (2007). The Grammar of Words: An Introduction to Morphology (Toleo la 2). Oxford: Oxford University Press.
- TUKI (1990) kamusi sanifu ya Isimu and Lugha, Dar Es Salam: TUKI.
- Richard, J.C., Platt, J. na Weber, H. (1985). Longman Dictionary of Applied Linguistics. London: Longman.
- Hartman, R.(1972) Dictionary of Language and Linguistics, London: Applied Science Publisher.
- Mohamed, A.M.(1986) *Sarufi Mpya*. Nairobi: Foundation Publishers.
- Mathews P.H (1997) Morphology (Toleo la 2): An Introduction to the Theory of Word Structure. Cambridge: Cambridge University Press.
- Crystel, D.(1971) Linguistics. Middlesex:Penguin.
- TUKI. (2013). Kamusi ya Kiswahili Sanifu (Toleo la 3). Nairobi: Oxford University Press.
- Nida, E.A. (1949). Morphology: The Descriptive Analysis of Words (Toleo ya 2). Ann Arbor: The University of Michigan Press.
- Weber,H. (1985). A Dictionary of Phonetics and Linguistics. Harlow Longman.
- Elishafati J. Ndumiwe na Tasiana Jasson (2022) *Matumizi ya Kanuni za Utambuzi wa Mofimu za Nida (1949) katika Utambuzi wa Mofimu za Lugha ya Kiswahili,* Kioo cha

Lugha, Juz. 20(1), 100-114 Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v20i1.7 Kioo cha Lugha, Juz. 20(1), Juni.

- https://askfilo.com/user-question-answers-smart-solutions/swali-la-tatu-i-fasili-dhana-mofimu-mofu-na-alomofu-alama-7-3434393036393739.
- https://www.google.com/search?q=uhwiano+baina+mofu+na+mofimu&rlz=1C1CHBF_enTZ847TZ847&oq=uhwiano+baina+mofu+na+mofimu&gs_lcrp=EgZjaHJvbWUyCwgAEEUYChg5GKABMgkIARAhGAoYoAHSAQoyNDA2MWowajE1qAIIsAIB8QXO2OB,Y4j7mA&sourceid=chrome&ie=UTF-8.